# KITUO CHA MAFUNZO YA VIWANDA VYA MAZAO YA MISITU NA MBAO , MAFINGA

PANDA MITI KIBIASHARA
PRIVATE FORESTRY PROGRAMME

## Utangulizi

Kukosekana kwa ngazi thabiti ya huduma za mafunzo ya ufundi stadi imekuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo ya viwanda vya misitu na vya mbao ndani ya nyanda za juu kusini, licha ya ukweli kwamba eneo hili ndio kitovu cha viwanda vya misitu na vya mbao nchini Tanzania.

Programu ya Panda Miti Kibiashara imeanzisha **Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazao ya Misitu** ili kuziba pengo hili. Kituo hiki kilifunguliwa rasmi tarehe 1 Desemba, 2017 na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii mheshimiwa Japhet Hasunga.

Kituo kinatoa wigo mpana wa huduma kuanzia mafunzo kwa vitendo katika mambo yote yanayohusu misitu, kusaidia na kushauri mipango ya kibishara, utawala na maendeleo. Huduma za ziada zikiwemo za uendelezaji wa bidhaa, huduma za ununuaji mashine, kujenga mtandao na kutafuta fedha kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza biashara zinazohusiana na misitu.







## Kanuni za mafunzo za Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazao ya Misitu

### Mafunzo kwa vitendo yatakayokuhakikishia ujuzi

Mafunzo yote yanayoandaliwa na kituo hiki ni mafunzo ya vitendo yanayokupa ujuzi muhimu unaokuwezesha kufanya kazi kwa usahihi na uangalifu. Nadharia hutumiwa katika maeneo muhimu tu, kwakuwa muda mwingi wa mafunzo umetengwa kwa ajili ya mazoezi chini ya usimamizi.

### Wakufunzi wenye ujuzi na wenye uzoefu wa miaka mingi katika mafunzo kwa vitendo

Wakufunzi wetu wote wamebobea katika mafunzo kwa vitendo na wenye uzoefu wa miaka mingi katika fani hii. Watakusaidi kuainisha mahitaji yako katika kuboresha seti ya ujuzi, huku wakikuhamasisha kuukubali wezo wako. Kozi zetu zinalenga ukamilifu wa mada ya kozi pamoja na taaluma huku umakini ukiwekwa katika ujuzi muhimu.

### Usalama kwanza

Kozi za ufundi za kituo zinajumuisha matumizi ya vifaa vya kujilinda na madhara kazini na zinazingatia kanuni za usalama na afya mahali pa kazi. Mafunzo yote yanasimamiwa na mtaalamu wa usalama na afya mahali pa kazi anaehakikisha usalama wako wakati wa mafunzo. Kozi za kiufundi zinahusisha mafunzo ya utawala na mipango ambayo unaweza kuyatumia kazini katika usalama na afya mahali pa kazi .

### Ushirikiano wa timu

Kozi zote zinahusisha idadi kubwa ya kazi za makundi ili kuhakikisha unajifunza namna ya kutumia mbinu mpya ulizojifunza. Hivyo, utakaporudi kazini utafahamu namna ya kufundisha na kusaidia wengine. Hii inahakikisha matumizi sahihi ya muda na fedha zinazohitajika kwenye mafunzo na kujifunza kwa kuendeleza matokeo chanya mahali pote pa kazi.





*Hapa unamwona mmoja wa wakufunzi akionesha matumizi sahihi ya vifaa vya kujikinga na ajali wakati wa uvunaji: kofia, viziba masikio na kioo (vinachoshushwa kukinga masikio na macho wakati wa kuangusha miti), vesti ya usalama na suruali (iliyo na ngao ya kuzuia miguu usiathiriwe na wembe wa msumeno wakati inapotokea ajali), glavu na buti za kujikinga na ajali. Ni muhimu wavunaji waonekane wakati wa shughuli za kuvuna, hata kama eneo limefungwa kutumika.*





## Mtaala wa kozi

### Kozi za Utawala, Usimamizi na Ujasiria mali

- Ujuzi wa msingi katika teknolojia ya habari
- Ujuzi wa juu katika teknolojia ya habari
- Misingi ya afya na huduma ya kwanza katika misitu na viwanda vya mbao
- Misingi ya juu ya afya na huduma ya kwanza katika misitu na viwanda vya mbao
- Ujuzi wa mawasiliana na mawasilisho
- Utangulizi katika ujasiriamali na biashara
- Usimamizi wa biashara
- Masoko
- Uhifadhi wa vitabu vya fedha na uhasibu
- Usimamizi wa fedha
- Mpango na usimamizi wa biashara ndogo ndogo na za kati (SME)
- Ustadi wa usimamizi na uongozi

### Kozi za Misitu

- Kazi za misitu na mipango ya fedha
- Uanzishwaji wa vikundi vya wakulima wa miti (Tree Growers' Association)
- Usimamizi wa vikundi vya wakulima wa miti
- Kusimamia afya na usalama wa kazi katika shughuri za misitu
- Kuhakikisha afya na usalama wa kazi katika shughuri za misitu
- Matengenezo ya msingi: matengenezo ya vifaa vya kujizuia vya msituni, mashine na vifaa vingine
- Matengenezo ya juu: kusimamia matengenezo ya vifaa vya kujikinga, zana za misitu, mashine na vifaa
- Uanzishaji wa kitalu cha miche ya miti
- Usimamizi wa kitalu cha miche ya miti
- Uanzishwaji wa mashamba ya miti na usimamizi wa miti michanga
- Usimizi wa shamba la miti lenye miti iliyokomaa (kupogoa, kupunguza na kuvuna)
- Takwimu za misitu
- Uzuiaji na uthibiti wa moto kichaa
- Mafanikio ya kizazi asilia
- Utengenezaji wa mkaa

### Kozi za uchakataji mbao

- Matengenezo ya kisu cha msumeno wa magogo ya kipenyo kikibwa
- Matengenezo ya kisu cha msumeno mduara
- Mipango ya uzalishaji katika viwanda vya mbao
- Uchanaji mbao kwa uthibiti wa upotevu wake kwa kuongeza thamani ya mbao
- Ufanisi, uzalishaji, na uchumi katika uendeshaji viwanda vidogo na vya kati (SMEs)
- Utunzaji wa kumbukumbu katika biashara ya kiwanda cha mbao
- Ukaushaji wa mbao kwa msimu kwa kutumia hewa
- Msumeno wa magogo makubwa na urekebishwaji wa pitio la gogo
- Msumeno mduara na uchakataji wa marudio
- Upasuaji wa magogo kwa msumeno wa magogo makubwa na uchakataji wa marudio
- Utunzaji, urekebishaji patio la gogo na uainishaji ubovu wa msumeno mduara na msumeno wa magogo makubwa
- Udhibiti wa ubora katika shughuli za uchakataji mbao
- Mahitaji ya ubora, thamani na matumizi ya malighafi
- Usalama katika viwanda vya mbao
- Ukataji kingo na upunguzaji ubao
- Uchambuzi na uwekaji mbao katika makundi ya viwango
- Utangulizi wa ukaushaji mbao kwa tanuru katika shughuli za uchakataji mbao ndani ya viwanda vidogo vidogo na vya kati
- Uhifadhi wa mbao
- Tekinolojia ya kaboni na stellite katika unoaji misumeno

### Huduma za ziada zitolewazo na kituo

Ukiacha ubora wa juu wa elimu ya mafunzo unaotolea, kituo kinatoa huduma na ushauri katika mambo yafuatavyo;

- Maelezo ya mashine
- Mchakato wa maendeleo
- Mpango wa biashara
- Usimamizi na uendelezaji biashara

Pia chuo kinatoa msaada katika hatua za uagizaji na ununuaji mashine, kutengeneza mtandao na kutafuta vyanzo vya mapato kwa ajili ya uanzishaji na uendelezaji biashara. Kituo kinaweza kutumika katika kuandaa warsha, matukio mbalimbali pamoja na mikutano na wateja.

### Mawasiliano na namna ya kufika kituoni


Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazeo ya Misitu (KMVMM)

Kinyanambo

Mafinga

Mr. Edigary, Mwaifweya Meneja wa Kituo.

Barua pepe: edigary.mwaifweya@privateforestry.or.tz

Tel: +255 744 874 521


Maelezo kwa watumiaji magari: Njia panda ya kituo cha Mafuta cha CF, barabara iendayo Madibira, endesha umbaki wa kilomita moja. Utaona kibao cha kituo upande wa kushoto mwa barabara, mkabala na kiwanda cha mkaa.

### Kuhusu Programu ya Panda Miti Kibiashara PFP)

Pandamiti Kibiashara husaidia umiliki binafsi wa mashamba ya miti hasa katika uanzishwaji na utunzaji wa mashamba ya miti kwa wakulima wadogo, kadhalika viwanda vya mazao ya misitu pamoja na ukuaji wa soko la mazao ya mbao yaliyokomaa ambayo yatanufaisha wadau wote. Programu inatekeleza katika Mikoa minne: Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma.


Mradi unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finaland na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania.

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

FORMIN.FINLAND.FI
MINISTRY FOR FOREIGN AFFAIRS OF FINLAND


© Private Forestry Programme 2018